# Historia Fupi ya Maisha ya Bahá'u'lláh



## Bahá'u'lláh

**(Utukufu wa Mungu)**

# Historia Fupi ya Maisha ya Bahá'u'lláh

*Kijitabu hiki kimeandaliwa maalum kwa ajili ya Maadhimisho ya Siku Kuu Pacha ya Kuzaliwa kwa Báb na Miaka Mia Mbili ya Kuzaliwa kwa Baha'u'lláh, na kuchapishwa na:*

*Kamati ya Vitabu, Uchapishaji na Usambazaji*
*ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*
*S.L.P. 585, Dar Es Salaam, Tanzania.*
*Barua Pepe: secretariat@bahai.or.tz*
*literature@bahai.or.tz*

*Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili na:*

*Kamati ya Uhakiki wa Tafsiri ya Kiswahili ya Kitaifa*
*ya Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

*© Baraza la Kiroho la Kitaifa la Wabaha'i wa Tanzania*

*Toleo hili la Pili: 2019*

***“Ufunuo ambao, kutoka zama zisizokumbukika, umetangazwa kama kusudi na ahadi za Mitume wote wa Mungu, na shauku iliyohifadhiwa kwa upendo mno wa Mitume Wake, sasa kwa ajili ya Mapenzi yaeneayo pote ya Mwenyezi na kufuatana na amri Yake isiyozuilika, umefunuliwa kwa watu. Ujio wa Ufunuo kama huo umetangazwa katika Maandiko yote Matakatifu.”*** **-** *Bahá’u’lláh*



***Ee wewe unayengojea, usiendelee kukawia, kwani amekuja. Angalia nyumba yake takatifu na utukufu wake ukikaa humo ndani. Ni utukufu wa kale, ukiwa na ufunuo mpya.***
*Baha’u’lláh*

## Kuzaliwa na Maisha Yake ya Mwanzoni

Mirza Husayn Ali, ambaye baadaye alijulikana kwa jina la Baha'u'lláh (Utukufu wa Mungu), Alizaliwa Tehrán, mji mkuu wa Uajemi, alfajiri ya 12 Novemba, 1817. Alikuwa mtoto wa kiume wa kwanza wa Mirza Abbás Burzúg-Núr aliyekuwa mmoja wa mawaziri katika baraza la Sháh (Mfalme wa Uajemi). Ukoo Wake ulikuwa tajiri na maarufu sana nchini humo. Baha'u'lláh hakwenda shule, elimu Yake ndogo aliipata nyumbani.

Tangu utotoni, Yeye alikuwa na tabia za kipekee sana. Alikuwa mtulivu, mwema na mkarimu kupindukia. Alipenda sana madhari ya asili, alitumia muda Wake mwingi bustanini na mashambani. Alikuwa na uwezo wa ajabu na wa kuvutia ambao ulitambuliwa na wote, hivyo kupendwa na kila mmoja. Daima watu walimzunguka kwa wingi, wakiwemo mawaziri, wajumbe wa baraza, na hata watoto wadogo. Alipokuwa na umri wa miaka kumi na mitatu au kumi na minne hivi, alisifiwa sana kwa maarifa na uwezo wa akili Yake ya asili. Angeweza kuongea juu ya jambo lolote na kutatua tatizo lolote gumu lililotolewa Kwake, akijitosa katika mikusanyiko mikubwa kujadili mambo mazito pamoja na walimu mashuhuri wa dini na kufafanua maswali magumu ya kidini. Wengi walimsikiliza kwa makini.

Alipotimiza umri wa miaka ishirini na miwili, baba Yake alifariki, akimwachia majukumu ya kuwatunza ndugu na dada Zake wadogo na kusimamia mashamba makubwa ya ukoo wao. Serikali ilimtaka arithi cheo cha baba Yake kama ilivyokuwa desturi nchini Uajemi, lakini Yeye alikataa. Waziri mkuu akasema: ***"Mwacheni peke yake. Nafasi kama hiyo haimfai. Ana shabaha kubwa zaidi mbele yake. Mimi siwezi kumuelewa, lakini nina hakika kwamba amekusudiwa kwa ajili ya kazi bora zaidi. Mawazo yake siyo kama yetu. Mwacheni peke yake."***



*Nyumba ya Baha'u'lláh huko Tehrán, Irán*

## Afungwa Jela kama Mfuasi wa Báb

Báb (Mtangulizi wa Baha'u'lláh) alipotangaza utume Wake mwaka 1844, Baha'u'lláh, ambaye wakati huo alikuwa na umri wa miaka ishirini na saba, aliinuka kuiunga mkono na kuieneza kwa ujasiri, uthabiti na ushupavu hoja ya Imani hii mpya.

Alikuwa ameshafungwa gerezani mara mbili kwa ajili ya Imani hiyo, na wakati fulani aliteswa vikali kwa kuchapwa kwenye nyayo, kufuatia jaribio la hatari lililofanywa na Sadiki (mmoja wa wafuasi wa Báb), Agosti 1852 ambaye alidhamiria kumuua mfalme (Sháh) ili kulipiza kisasi kutokana na mauaji ya kutisha ya Bwana wake mpendwa (Báb). Yeye mwenyewe alikamatwa na kuuawa papo hapo. Wabáb wengi walikamatwa, kuteswa vikali na themanini kati yao waliuawa mara moja mjini Tehrán, na wengine kurundikwa magerezani, akiwemo Baha'u'lláh. Walifungwa katika Gereza la Siyáh-Chál kwa miezi minne. Usiku mmoja katika ndoto, maneno haya matukufu yalisikika kila upande: ***"Kweli, tutakufanya mshindi wewe mwenyewe na kwa kalamu yako. Usihuzunike kwa yaliyokupata, wala usiogope kwani u salama. Muda si mrefu Mungu atatoa tunu za dunia-watu watakaokusaidia kwa njia yako na kwa njia ya jina lako, ambalo kwalo Mungu ameiamsha mioyo ya watu wale ambao wamemtambua."***



*Gereza la Siyáh-Chal(Shimo Jeusi)*



*Pingu ya mbao iliyotobolewa*



***Mnyororo aliofungwa Baha'u'lláh shingoni***

## Uhamishoni

## Baghdád

Licha ya kifungo hiki cha kutisha kilichodumu kwa miezi minne, Baha'u'lláh na wafuasi Wake waliendelea kuwa na moyo wenye juhudi na furaha kubwa. Karibu kila siku mtu mmoja au wawili kati yao aliteswa au kuuawa. Yule ambaye jina lake liliitwa alitamani kucheza ngoma. Kwa furaha aliibusu mikono ya Baha'u'lláh, kuwakumbatia wenzake, kisha aliharakia kwa shauku na furaha kwenda kuuawa. Ilithibitika dhahiri kwamba Baha'u'lláh hakuhusika na mipango ya kumdhuru mfalme, hata waziri wa Kirusi alishuhudia kuhusu usafi wa tabia Yake. Kwanza Yeye alikuwa mgonjwa hivyo asingeweza kufanya hivyo. Hivyo, badala ya kumpa hukumu ya kifo, Sháh aliamuru ahamishwe na kupelekwa Mesopotamia huko Iráq; majuma mawili baadaye, Baha'u'lláh aliondoka, akiambatana na jamaa Zake na baadhi ya waumini wengine, wakitaabika sana kwa

baridi na shida zingine katika safari yao ndefu iliyofanywa majira ya baridi kali, na wakawasili mjini Baghdád katika hali ya ufukara wa hali ya juu kabisa.

Mara tu baada ya kupata ahueni, Baha’u’lláh alianza kuwafundisha wale waliomtembelea, akiwahimiza na kuwashauri waumini, na hapo Wabábi wakajawa na amani, furaha na matumaini mapya. Walakini hali hii ilidumu kwa muda mfupi tu kwani Mirza Yahya (Subh-i-Azal), ndugu wa kambo wa Baha’u’lláh, aliwasili Baghdád na akaanza kuchochea mifarakano kisiri-siri. Tofauti hizi ambazo zilienea na kuleta ghasia hadi huko Adrianople zilimhuzunisha sana Baha’u’lláh ambaye nia yake maishani ilikuwa kudumisha umoja miongoni mwa watu wa dunia.




***Ramani kuonesha Uhamisho wa Bahá’u’lláh***

## Miaka Miwili Nyikani

Kama mwaka mmoja hivi baada ya kuwasili Bahgdád, Baha’u’lláh aliondoka peke Yake kwenda katika mapori ya Sulaymaniyyih (Kurdistán), bila kuchukua kitu kingine chochote isipokuwa nguo za kubadilisha. Kuhusu sababu ya kuondoka Kwake, Baha’u’lláh ameandika yafuatayo katika Kitabu cha Yakini (Kitab-i-Iqán) na hapa tunanukuu kwa ufupi tu:

***“….Kuondoka kwetu ilikuwa kuepuka tusiwe chanzo cha ugomvi kati ya waumini, asili ya mchafuko kwa wenzetu, njia ya maumivu kwa kiumbe yeyote, au sababu ya huzuni kwa roho yoyote…Tulikaa huko mpaka saa ile ambapo mwito wa***

***asili yake isiyojulikana ulipotokea na kutuamuru turudi kule tulikotoka. Tukitoa matakwa yetu kwake, tuliitikia agizo lake. Ni kalamu gani iwezayo kuelezea mambo tuliyoyaona tuliporudi nyumbani! Miaka miwili imepita na wakati huo maadaui zetu wameendelea kujaribu kwa juhudi kubwa kila hila ili kutuangamiza, ambapo wote washuhudia*** – Kitabu Iqan, uk. 250-252

## Upinzani wa walimu wa Kiislamu

Baada ya kurejea Kwake kutoka nyikani, sifa Yake iliongezeka kuliko hapo awali, watu kutoka nchi za mbali walimiminika jijini Baghdád kwenda kumuona na kusikiliza mafundisho Yake, Wayahudi, Wakristo, Wazoroasta, na hata Waislamu, walionekana kuujali utume huu mpya. Walakini, walimu wa kiislamu waliinua upinzani na wakazidi kufanya mipango ya hila ili kumuangamiza. Siku moja walimtuma mmoja wao ili kumuuliza Baha’u’lláh maswali fulani. Mjumbe huyu aliona majibu ya Baha’u’lláh ni ya kuridhisha mno na hekima Yake ni ya kustaajabisha mno. Walakini, ili kwenda kuwaridhisha wale waliomtuma alimuomba afanye muujiza kama thibitisho. Baha’u’lláh alimpa masharti kuwa atafanya hivyo tu ikiwa wangesaini kuwa baada ya kufanya hapo wangekiri ukweli wa utume Wake. Waliogopa na wakaamua kuachana na shauri hilo.

Basi, jinsi Baha’u’lláh alivyokuwa wa namna ya kipekee, wakati wa msukosuko huu, serikali ya Uajemi na Uturuki zilipokuwa zikifanya juhudi za pamoja ili kuiangamiza harakati hii kwa kuchochewa na walimu wa kiislamu, na balozi wa Uajemi mjini Baghdád, Yeye alikaa kwa utulivu na ukunjufu, akiwatia moyo na kuwafariji wafuasi Wake na kuandika maneno ya kudumu ili kuleta faraja na uongozi.

## Tangazo katika Bustani ya Ridván huko Baghdád

Serikali ya Uajemi na serikali ya Uturuki iliamua kuwa Baha’u’lláh ahamishiwe Contantinople. Wafuasi Wake walishikwa na hofu kwa taarifa hii. Wageni walifurika makundi kwa makundi hata ikalazimu Familia Yake kuweka mahema

katika Bustani ya Najib Pasha, nje kidogo ya Jiji la Baghdád kwa muda wa siku kumi na mbili, kama maandalizi ya safari hiyo ndefu. Hii ilikuwa ni kuanzia April 21 hadi Mei 2, 1863, miaka kumi na tisa kamili tangu Tangazo la Báb. Ni akiwa katika Bustani hii ambayo imeitwa na Wabahá'i ***"Bustani ya Ridván"*** ambapo Baha'u'lláh aliwatangazia wafuasi Wake kwamba Yeye Ndiye Yule Ambaye kuja Kwake Báb, mteule wa Mungu alikutabiri pamoja na Manabii wote. Siku alizokaa humo zinaadhimishwa kila mwaka kama ukumbusho Wake na inajulikana kama ***"Siku Kuu ya Ridván."***



***Madhari ya Bustani ya Ridván – Akká***

## Contantinople na Adrianople

Safari ya Constasntinople (Instanbul) ilichukua kati ya miezi mitatu na minne, wasafiri wakiwa ni Baha'u'lláh, jamaa Zake na wafuasi ishirini na sita. Huko walifungwa katika nyumba ndogo ambamo walisongamana mno, baadaye walipewa nyumba nzuri kidogo. Baada ya miezi minne walihamishwa tena kwenda Adrianople (Edirne). Safari ya hii ingawa ilichukua muda mfupi, ilikuwa ya kutisha zaidi kuliko zote walizopata kusafiri. Theluji ilianguka kwa wingi karibu wakati wote na kwa kuwa hawakuwa na nguo wala chakula cha kutosha, mateso yao yalipindukia. Majira ya baridi kali Baha'u'lláh na jamaa Zake, jumla yao wakiwa kumi na wawili, waliwekwa katika nyumba ndogo yenye vyumba vitatu, iliyojaa wadudu. Baadaye walipewa nyumba nzuri kidogo. Walikaa huko Adrianople kwa zaidi ya miaka minne na nusu. Hapa Baha'u'lláh alianza tena kufundisha na akawa na wafuasi wengi. Wabáb wengi


walikubali kwa shauku na tangu wakati huo walijulikana kama Wabahá'i. Walakini, wachache chini ya uongozi wa Mirza Yahya, walimpinga vikali na mateso makubwa yakafuata. Hatimaye serikali ya Uturuki iliamua kuwahamisha wote; Wabáb na Wabahá'i, Baha'u'lláh na wafuasi Wake walipelekwa Akká, Palestine (Israel), na Mirza Yahya na kikundi chake walipelekwa Cyprus.

## Barua kwa Wafalme

Ni katika kipindi hiki ambapo Baha'u'lláh aliandika barua zenye nguvu kwa wafalme na watawala mbalimbali wa dunia. Baadaye, katika "Kitab-i-Aqdás, maneno yake yaliandikwa kwa ajili ya wafalme wengine, watawala na marais wa Marekani, viongozi wa dini kwa jumla na binadamu wote, akiwasihi kutumia nguvu zao kwa ajili ya kusimamisha dini ya kweli, serikali ya haki na amani kati ya mataifa. Katika barua Yake kwa Sháh, Baha'u'lláh alitetea kwa nguvu kisa cha Wabábi waliokuwa wakiteswa na akaomba apewe nafasi ya kukabiliana uso kwa uso na wale waliochochea na kuleta mateso hayo, lakini hakukubaliwa. Katika barua hiyo, Baha'u'lláh alionesha kuhuzunishwa, Kwake na mateso ya Wabáb na matumaini Yake kwa siku zijazo. Hapa ni sehemu tu ya barua hiyo:

***Ee mfalme, Mimi nimeona katika njia ya Mungu kile ambacho hakijaonekana na jicho lolote wala kusikiwa na sikio lolote. Marafiki wamenikana; njia zenye mashaka zinaelekezwa Kwangu; dimbwi la usalama limekauka kabisa; uwanja wa faraja umeunguzwa…Ni misiba mingapi imeshuka na mingapi itashuka! Natembea nikisonga mbele kuelekea kwa Mwenyezi…ambapo nyuma Yangu nyoka ananinyemelea, macho Yangu yakibubujikwa na machozi mpaka kitanda changu kinaloa…Kwa jina la Mungu, kichwa Changu kinatamani mikuki ya upendo wa Bwana Wake…Naam, kwa sababu nawaona binadamu wakipotea katika ulevi wao, nao hawajui; wametukuza tamaa zao mbaya na kumweka kando Mungu…na kuiona amri ya Mungu kama mzaha, mchezo na upuuzi…hakika kesho watakiona kile wanachokikana sasa. Sasa tupo karibu kuondolewa mahali hapa pa mbali***

***tulipohamishiwa (Adrianople) na kupelekwa jela ya Akká. Na wasemavyo wengine, hakika ni mji wa ukiwa na usiopendeza kuliko mingine yote ulimwenguni, mji wenye hali ya kuchukiza mno na maji ni machafu mno…Na humo ndimo wanamokusudia kumfungia Mtumishi huyu, na kufunga mbele ya macho Yetu ile milango ya huruma na kutunyang'anya mambo mazuri ya maisha yetu…Natumaini kwa neema Yake (Yeye ni Mtukufu)…kwamba atazigeuza nyuso za watu wote ziwe za kweli kuelea Kwake…Na tunamuomba kuufanya msiba huu mbaya kuwa ngao ya shirika la watakatibu Wake…"***



**Mstari wa kwanza:** ***Nasiri'd-Din Shah (Uajemi), Sultan Abdul-Aziz (Ufalme wa Ottoman), Tzar Nikolaevitch Alexander II (Urusi), Kaiser William I (Ujerumani)***
**Mstari wa pili:** ***Mfalme Francis Joseph (Austria-Hungary), Mfalme Napoleon III (Ufaransa), Malkia Victoria (Falme za Uingereza), Papa Pius IX (Kanisa Katoliki).***

## Kifungoni Akká

Wakati huo gereza la 'Akká lilikuwa gereza walikopelekwa wale waliofikiriwa kuwa ni waovu kabisa kutoka sehemu zote za milki ya Uturuki. Baada ya kuwasili huko, Baha'u'lláh na wafuasi Wake, jumla wakiwa kati ya watu themanini na themanini na wanne, wakiwemo wanaume, wanawake, na watoto, walifungwa katika kambi ya kijeshi. Palikuwa pachafu

mno, hakuna vitanda, chakula walichopewa kilikuwa duni sana na hakikuwatosha kamwe. Baadaye waliomba waruhusiwe kujinunulia chakula chao wenyewe. Homa ya malaria, kuhara damu n.k. ikazuka, na wote isipokuwa wawili tu, wakawa wagonjwa. Watatu kati yao walifariki.

Kifungo hiki kikali kilidumu kwa zaidi ya miaka miwili, na hakuna yeyote miongoni mwa Wabahá'i aliyeruhusiwa kutoka nje ya lango la gereza, isipokuwa wanne tu ambao walichungwa kwa uangalifu walipokuwa wakitoka kila siku kwenda kununua chakula. Wageni walikatazwa kabisa kuwaona. Wale waliosafiri kwa miguu kutoka Uajemi kwenda kumuona Kiongozi wao Mpendwa, waliishia nje tu. Iliwalazimu kusimama mahali fulani ambako waliweza kumuona na kupungiana mikono na Baha'u'lláh kupitia dirisha la chumba Chake. Kasha wangelia na kuanza safari kurudi nyumbani kwao wakiwa wametiwa moyo.



***Gereza la Akká alimofungwa Baha'u'llah***



***Mandhari ya Gereza la Akká likitazamana na Bahari ya Mediterrania***

## Vizuizi vyalegezwa

Walipokuwa katika gereza la Akká Mirzá Mihdi (mtoto wa Baha'u'lláh) alianguka kutoka ghorofani hadi chini wakati alipokuwa akitembeatembea huku akiwa amezama katika sala na tafakari ambapo mbao zilimchoma mbavuni. Baha'u'lláh alimuuliza kama angependa amponye lakini yeye alisema angependelea zaidi kuyatoa dhabihu maisha yake ili wafuasi Wake waruhusiwe kuingia machoni Pake. Hivyo Mirzá Mihd akakata roho.



***Mirza Mihd***

Muda si mrefu, hali ya kifungo ilianza kulegezwa. Baha'u'lláh na jamaa Zake walihamishiwa katika nyumba yao peke yao na wenzao wakapewa nyumba nyingine. Baha'u'lláh alifungwa hapa kwa miaka saba zaidi. Katika chumba kidogo karibu na kile alimofungiwa, ndugu Zake kumi na watatu, wake kwa waume, iliwalazimu kujihifadhi! Tangu wakati Baha'u'lláh na wafuasi Wake walipoondoka kwenye makao ya jeshi, wageni waliruhusiwa kuwatembelea, na pole pole amri kali zilizowekwa na mfalme zikasahauliwa moja baada ya nyingine.

## Milango ya Gereza Yafunguliwa

Hata wakati ule kifungo kilipokuwa kikali zaidi Wabahá'i hawakufadhaika na imani yao tulivu haikudhoofika kamwe. Walipokuwa kwenye makao ya jeshi huko 'Akká, Baha'u'lláh aliwaandikia marafiki Zake hivi: ***Msiogope. Milango hii itafunguliwa. Hema langu litapigwa juu ya mlima Carmeli na itakuwa furaha kuu.*** Tamko hili lilileta matumaini na faraja kubwa kwa wafuasi Wake, na muda si mrefu likatimia. Baadaye 'Abdu'l-Bahá aliandika kisa cha jinsi milango ya gereza ilivyofunguliwa, (rejea Baha'u'lláh na Wakati Mpya kuanzia uk.21).

## Maisha huko Bahji

Tangu mwanzo na hata maisha Yake ya baadaye Baha'u'lláh alionesha jinsi ya kumtukuza Mungu katika hali ya umasikini na fedheha. Huko Bahji, alionesha pia jinsi ya kumtukuza Mungu

katika hali ya heshima na neema. Maisha ya Mkamilifu huyu aliyebarikiwa pamoja na jamaa Zake yalikuwa ya kawaida sana. Anasa na ubinafsi vilikuwa mwiko katika nyumba Yake. Karibu na nyumba Yake waumini walilima bustani nzuri iliyoitwa **"Ridván"** ambayo mara nyingi alitumia siku nyingi akilala humo. Alitembelea huko Akká na Haifa, mara chache akipiga hema Lake juu ya mlima Carmeli nje ya lango la kuingilia pango la Eliya kama Eliya mwenyewe alivyotabiri na kama alivyotabiri Bah'u'llah alipokuwa kifungoni mjini Akká. Ni katika kipindi hiki ambapo Yeye alimuonesha 'Abdu'l-Bahá mahali pa kujenga Kaburi Takatifu la Báb juu ya Mlima huu wa Mungu.

Baha'u'lláh alitumia muda Wake mwingi akisali na kutafakari, kuandika vitabu vitakatifu, kufasiri maandiko mengine na kuwapa marafiki mafundisho ya kiroho. Ili kumpa nafasi kwa ajili ya kazi hii kuu, Abdu'l-Bahá alisimamia shughuli zingine zote k.v.  kukutana na walimu wa kiislamu, watunga mashairi na maafisa wa serikali waliopendezwa na kufurahishwa sana Abdu'l-Bahá. Ingawa hawakuwa wamekutana na Baha'u'lláh Mwenyewe kwa kujuana kwao tu na mwanaye waliingiwa na moyo wa kirafiki kwa Baha'u'lláh kwani kupitia Abdu'l-Bahá walilielewa daraja la Baba Yake.

## Kupaa kwa Baha'u'lláh

Baha'u'lláh alifariki dunia (alipaa) mnamo 29, Mei,1892, akiwa na umri wa miaka sabini na tano (75) kutokana na homa ya kawaida na kuzikwa huko Bahji, Israel (Nchi Takatifu). Kufariki na kuzikwa Kwake huko Bahji, Israel kunatimiza unabii usemao: ***"Na Sharon itakuwa zizi la makundi, na bonde la Akká litakuwa mahali pa mifugo kujilaza, kwa watu wangu***



***Kaburi Takatifu la Bahá'u'lláh – Bahji, Israel***

Siku tisa baada ya kifo Chake, kisanduku kilichokuwa na hati fupi ya Wasia kilivunjwa na mwanaye mkubwa mbele ya ndugu Zake na marafiki wachache na kubainika kuwa 'Abdu'l-Bahá, mwanaye mkubwa wa kiume aliteuliwa kuwa Mrithi na Mfasiri Pekee wa Maandiko Yake.

## Ujumbe Wake

Msingi wa Ujumbe wa Baha'u'lláh duniani ni Umoja----umoja Mungu, Umoja wa Dini na Umoja wa binadamu wote. Yeye anasema: ***"Ninyi ni matunda ya mti mmoja na majani ya tawi moja. Mtu asijivunie kwamba anependa nchi yake, bali ni afadhali ajivunie kwamba anapenda aina yake."***

Manabii waliotangulia wamehubiri kuja kwa amani kuu duniani na upendo miongoni mwa watu, nao wametoa maisha yao ili kuharakisha kuja kwa mambo hayo, kila mmoja wao akitamka wazi kwamba hali hii itafikiwa tu katika kipindi cha ***"kuja kwa Bwana"*** ambapo wabaya watahukumiwa na waliowema watatuzwa.

Musa alibashiri juu ya uhamisho, mateso na dhuluma kwa wana wa Israeli kabla ya kutokea kwa bwana wa majeshi kuwakusanya kutoka mataifa yote, kuwaangamiza wale wadhalimu na kusimika ufalme wake hapa duniani.

Kristo alisema "msifikiri kuwa mimi nimekuja kuleta amani duniani la, bali upanga" (Mathayo x ,34) na akatabiri muda wa vita na uvumi wa vita, wa taabu na mashaka, ambao

ungeendelea mpaka kuja kwa mwana wa mtu" katika Utukufu wa Baba"

Muhammad alitamka kwamba, kwa sababu ya makosa yao, Mungu aliweka uadui na chuki miongoni mwao ambao ungeendelea hadi siku ya kiyama ambapo angetokea kuwahukumu wote.

Baha'u'lláh ametangaza kwamba Yeye Ndiye Yule aliyeahidiwa na Manabii wote hawa-Mdhihirishaji Mtukufu ambaye katika wakati Wake utawala wa amani utasimikwa hasa. Tamko hili halina mfano na ni la pekee sana, lakini hata hivyo linakubaliana kiajabu na ishara za nyakati zenyewe na tabiri za Manabii wote wakuu. Tangu kutokea kwa Baha'u'lláh hadi sasa, kumekuwa na vita na maangamizi makubwa mno, lakini haya ndiyo Manabii wote walitabiri kuwa yangetokea mwanzoni mwa "Siku ile kuu na ya kutisha ya Bwana", kwa hiyo ni uthibitisho wa maoni kwamba "kuja kwa Bwana" siyo kwamba kumekaribia tu, bali tayari. Inawezekana bado kuna matukio ya maafa ya kutisha duniani, lakini Baha'u'lláh anatuhakikishia muda si mrefu, mapigano haya yasiyo na faida na vita hivi vya maangamizi lazima vikome kabisa katika uso wa dunia.

## Maandiko Yake

Maandiko ya Baha'u'lláh yana mambo mengi yanayogusa kila sehemu ya maisha ya mwanadamu; mmoja mmoja na jamii kwa jumla - yenye fasiri ya Maandiko Matakatifu ya kale na ya siku hizi na yenye utabiri wa matazamio ya siku zijazo. Usahihi wa maarifa yake ulistaajabisha. Aliweza kufafanua kwa uthabiti na usahihi bila shaka yoyote Maandiko Matakatifu ya dini zilizotangulia.

Alitumia lugha ya Kiajemi na Kiarabu. Nyakati nyingine, kama wakati alipowaandikia Wazoroasta wenye elimu, alitumia Kiajemi safi, bora na cha kisasa kabisa. Pia aliandika Kiarabu kwa ufasaha, mara kwa mara akitumia lugha rahisi, na mara nyingine kwa mtindo wa ufasaha mwingi uliofanana kidogo na ule wa Qurán. Ufundi wake halisi wa lugha hizi na mitindo mbali mbali ulikuwa wa ajabu mno.

Katika baadhi ya maandishi Yake, alitumia lugha ya kuelewa hata kwa waliokuwa wajinga kabisa. Mengine yamejaa mashairi mazuri, elimu kuu, mafundisho ya Muhammad, Zoroasta na ya Maandiko Matakatifu mengine, au maandishi na masimulizi ya Kiajemi na Kiarabu, ambayo ni watunga mashairi, wataalamu na wanazuoni pekee wangeweza kuelewa vyema uzuri wake. Na mengine yanahusu hali za juu zaidi za maisha ya kiroho na yanaweza kufahamika tu kwa wale ambao wamekwishapita katika hali zile za mwanzo.

Ni kwa sababu hii kwamba hata wale walioelimika na wastaarabu, watunga mashairi ya kiroho na waandishi mashuhuri. Hata baadhi ya viongozi wa wasufi na wa madhehebu mengine, na baadhi ya mawaziri ambao walikuwa waandishi, walivutiwa na maneno Yake.

**Moyo wa Kibahá'i**

Kutoka Akká, Baha'u'lláh aliiamsha kweli kweli nchi Yake ya asili (Uajemi); na hata dunia nzima. Moyo uliomsukuma Yeye na wafuasi Wake daima ulikuwa upole, adabu, uvumilivu, na nguvu ya juhudi za ajabu na uwezo mkuu kabisa. Moyo huu uligeuza hali ya binadamu na watu waliokubali mwongozo Wake kuwa viumbe vipya. Walijawa na upendo, imani, shauku na furaha, na majonzi yao yalikuwa kama vumbi tu.

Jambo la ajabu kuliko yote, ni kwamba mioyo yao ilijaa furaha kuu mno ya maisha mapya kiasi kwamba hawakuwa na mawazo ya chuki na kisasi kwa watesi wao. Waliachilia mbali matumizi ya nguvu kama njia ya kujikinga, na badala ya kusikitika juu ya yaliyowapata, walijiona wenye bahati kuliko wote kwa kuteuliwa kwao kupokea ufunuo huu mpya na mtukufu na kutoa dhabihu maisha yao wakitumaini katika ahadi ya mwenyezi Mungu kwamba Baha'u'llah ndiye malaika mkuu (Mikaeli) aliyeshuka na kiti cha enzi akiongoza jeshi la mbinguni kuushinda udhalimu wa dunia. Waliamini kwamba Mungu alikuwa amekuja kusimika Ufalme Wake hapa duniani. Baha'u'lláh alitangaza Utume Wake Mwenyewe kama Báb alivyotabiri. Kutokana na kazi za uaminifu za mtangulizi Wake

Mkuu, maelfu walikuwa tayari kumpokea kwa shangwe alipotokea, maelfu walitupilia mbali ushirikina na chuki, wakingojea kwa mioyo safi na roho kunjufu udhihirisho wa Utukufu wa Mungu ulioahidiwa. Umasikini, mateso, fedheha na minyororo havikuwa kikwazo cha kumtukuza wa Bwana wao.

**Baadhi ya unabii wa kutoka Biblia kumhusu Baha'u'lláh**

Kuna unabii mwingi uliotimizwa kwa kuja kwa Baha'u'lláh. Kwa mfano ule unaohusu kurudi kwa Kristo kama ulivyoandikwa na nabii Daniel. Unabii huu hutaja parapanda (baragumu) tatu ikihusisha kurudi Kwake ambapo parapanda ya kwanza ni kutokea kwa Mtume Muhammad (S.A.W), ambaye angekuwa shuhuda wa siku ya kiyama (siku ya mwisho). Zile parapanda (baragumu) mbili za mwisho za mfuatano wa karibu kama ilivyothibitishwa na Mtume Muhammad Mwenyewe kuwa siku hiyo ya kiyama kutatokea baragumu mbili ambazo hata hivyo ni moja tu ndiyo Báb na Baha'u'lláh: ***Ufunuo: 11 Na 12); Az-Zumar 39:69-70, Muhammad47:39, Al-Faatir 35:16, Al-Maaida 5:49, nk.***

Báb (Lango) na Baha'u'lláh (Utukufu wa Mungu) ambao huchukuliwa kama Wajumbe (Wadhihirishaji) Pacha walikuja kwa mfuatano wa karibu sana ambapo Báb alikuwa lango la Baha'u'llah. Báb aliwaambia wazi wafuasi Wake kuwa Yeye amekuja kuwaandaa watu kwa ajili ya ujio wa "Yeye Ambaye Mungu Atamdhihirisha" na kuwaasa wafuasi Wake kuwa tayari kumgeukia Yeye mara tu atakapojidhihirisha. Kuna unabii mwingi sana unaomhusu Baha'u'lláh baadhi ni kama ufuatao:

***"Atakapotoka katika jela atakuja kutawala"…(Muhubiri 4:14)***

Kutoka jela ya Akká Bahá'u'lláh aliandika barua zenye nguvu sana kwa wafalme na watawala wa ulimwengu waliokuwa na nguvu katika karne ile ya 19, akianzisha msingi wa jamii Yake ya ulimwengu kwa siku zijazo.

***"Na Sharon itakuwa zizi la makundi, na bonde la Akká litakuwa mahali pa mifugo kujilaza, kwa watu wangu ambao wamenitafuta." (Isaya 65:10).***

***". . . na bonde la Akká liwe mlango wa tumaini." (Hosea 2:15).***

***"Na utukufu wa Mungu ulikuja nyumbani kwa njia ya lango ambalo maelekeo yake ni Mashariki." (Ezekiel 43:4)***

Bahá'u'lláh, ambaye maana ya jina lake ni ***"Utukufu wa Mungu"*** au ***"Utukufu wa Bwana"*** alihamishwa kwenda Nchi Takatifu Palestina (sasa Israel) kutoka nchi Yake ya kuzaliwa, Uajemi (Irán) iliyopo mashariki mwa Israel. Kwa jinsi hii unabii wa Ezekiel ulitimizwa.

***"Nami nitaweka kiti changu cha enzi katika Elam, na nitaangamiza kutoka huko mfalme na wana wa kifalme, asema Bwana." (Yeremia 49:39).***

Siku hizo Elam ilikuwa sehemu ya milki ya Uajemi, ambalo ndilo jina la kale la Irán, nchi alikozaliwa Bahá'u'lláh. Wafalme na wana wa Kifalme waliotajwa katika utabiri huu ndio wale waliotumiwa barua na Bahá'u'lláh na ambao tumewataja hapo juu. Wengi walipuuza maonyo Yake, wakapoteza nguvu zao na falme zao zote zikaangamizwa. Nasaba za ufalme wa kina Napoleon, Hohenzollerns, Hapsburgs, Qajars, Uthman, na Romanoffs zote zimetoweka kabisa katika historia.

***"Katika siku hiyo atakuja (Mtume wa Mungu) pia kwenu kutoka Assiria (Assyria), na kutoka miji iliyoimarishwa kwa kuzungushwa na kutoka kwenye ngome mpaka mtoni, na kutoka bahari mpaka bahari, na kutoka mlima hadi mlima". (Mika 7:12)***

Wakati mmoja Uajemi ilikuwa sehemu ya Milki ya kale ya Assyria. Utabiri huu haukutimizwa kwa mapenzi Yake, bali akiwa mfungwa na mhamishwa. Bahá'u'lláh alihamishwa kutoka Constantinople hadi Adrianople na hatimaye akapelekwa kwenye mji wenye ngome kuu wa Akká. Bahá'u'lláh alihamishwa kutoka Bahari Nyeusi mpaka Bahari ya Mediterania, kutoka Mlima wa Sar-Galu nchini Iráq mpaka mlima Carmel nchini Israel. Kwa jinsi hii unabii huu ulitimizwa. Kurudi kwa Nabii (Mtume) wa Mungu hakumaanishi kimwili na jina lile lile bali kiroho. Yesu Mwenyewe aliwafafanulia wanafunzi Wake kuwa Yohana alikuwa ndiyo kurudi kwa Eliya ***MATHAYO: 17:10-13***. Hivyo pia aliweka bayana kuwa hata

Yeye hatarudi kwa jina lile lile na kitabu kile kile ***ISAYA 62:2; UFUNUO 3:12***.

Baha'u'llah hajatumia jina la Yesu, bali amekuja na jina jipya. Yeye Mwenyewe huandika: ***"Enyi Wayahudi! Kama mmedhamiria kumsulubisha kwa mara nyingine tena Yesu, Roho ya Mungu, niueni Mimi, kwa kuwa tena katika nafsi Yangu, amedhihirishwa kwenu...Ingawa jina langu si jina lake."***

Kwa nini sharti tumuamini Bahá'u'lláh na kumkubali? Je, haitoshi kumuamini Yesu Kristo? Bahá'u'lláh amefundisha kwamba Ufunuo wa Mungu ni endelevu. Ulimwengu unaweza kulinganishwa na shule ambamo kila daraja la maendeleo linalingana na mafundisho yaliyoendelea kulingana na kiwango cha uelewa wa binadamu ambaye daima anasonga mbele. Mafunzo yanayotolewa katika daraja au darasa moja hayafuti yale yaliyotolewa katika darasa lililopita bali yanaendeleza mbele elimu. Jambo hilo pia linaonekana katika dini, wakati dini moja inapotokea baada ya nyingine. Hii njia iliyotolewa na Mungu ijulikanayo kama ***"Ufunuo Uendeleao"*** inaweza kulinganishwa na ukuaji wa mti. Ua haliliharibu tumba na wala tumba kuharibu ua; ni hatua mbalimbali za ukuaji wa mti huo au ni kama kukua kwa mwanadamu.

### Sala Aliyofunua Báb Kwa Ajili Ya Bahá'u'lláh

**(***Hii ni sala ambayo Báb Mwenyewe huinukuu katika "Dalia'il-i-Sab'ih" kama maombi Yake wakati wa miezi Aliyokuwa mfungwa katika gereza la Mah-ku):*

**"Ee Mungu wangu! Jalia Kwake, kwa nasaba Yake, kwa familia Yake, kwa rafiki Zake, kwa wafuasi Wake, kwa ndugu Zake na kwa wakazi wote wa dunia mwangaza ambao utasafisha maono yao na kurahisisha kazi yao; jalia kwamba waweze kujitwalia kazi zilizo bora kabisa hapa na hata baadaye! Kwa kweli, hakuna kishindikanacho Kwako.**

**Ee Mungu wangu! Mpe uwezo ili Alete uhuishaji wa dini Yako na tia uhai kupitia Yeye katika kile ambacho umekibadilisha katika Kitabu Chako. Dhihirisha kupitia Yeye Amri Zako mpya, ili kwamba kupitia Yeye dini Yako iweze kuchanua tena! Weka mikononi Mwake Kitabu Kipya, kisafi na kitakatifu, ili Kitabu hiki kiweze kuwa huru kutokana na mashaka yote na pasiwepo wa kukibadilisha au kukiharibu.**

**Ee Mungu wangu! Ondoa kupitia wangavu Wako giza lote na kupitia ushuhuda wa uwezo Wake weka kando sheria za kale. Kwa fahari Yake ishindayo wote waangamize wale ambao hawakufuata njia za Mungu. Kupitia Yeye waangamize wadhalimu wote, komesha, kwa kupitia upanga Wako, mafarakano yote; futa kabisa, kwa kupitia Haki Yake, aina zote za ukandamizaji; wafanye watawala watiifu kwa amri Zake; Zitiishe himaya zote za ulimwengu kwa Himaya Yake!**

**Ee Mungu wangu! Mnyenyekeze kila mmoja atamaniye kumnyenyekeza Yeye; Waangamize maadui Zake wote; mkatae yeyote ambaye humkataa Yeye na mpumbaze yeyote ambaye hupindisha ukweli, kugomea amri Zake; ajibidiishaye kutia giza nuru Yake na kuondoa jina Lake!"**

**Kisha Báb aliongeza maneno haya:**

Rudia maombi haya mara kwa mara, ikiwa muda wa kuyaghani haya yote utakosekana, usishindwe kutaja japokuwa yale maneno ya mwisho:


***"Muwe macho kwenye siku Atatakapochomoza Yule Ambaye Mungu Atamdhihirisha kwa sababu sala hii imeshuka kutoka mbinguni kwa ajili Yake."***

## Agano na Wasia wa Baha’u’lláh

Hili ni Agano ambalo hufanywa kuhusiana na urithi wa madaraka ndani ya dini. Katika Imani ya Kibahá'í jinsi ambavyo Agano la **Baha’u’lláh** lilivyowekwa wazi inaonekana kuwa kama muundo bainifu wa kimsingi wa dini, na chombo chenye nguvu kabisa cha ulinzi wa umoja wa Imani ya Kibahá'í na wafuasi wake.

Wakati **Baha’u’lláh**, Mjumbe wa Mungu, alipoanzisha Imani ya Kibahá’i mwaka 1863, aliweka mfumo kwa ajili ya uunganishaji wa jamii ya binadamu, kwa kusimika utawala wa kipekee miongoni mwa dini kuu za ulimwengu. Upekee huu ni kwamba utawala katika Imani ya Kibahá’i ni wa kidemokrasia –hakuna ukasisi katika Imani ya Kibahá’i.

Hata hivyo ili kuiandaa jumuiya ya Kibahá’i kuelekea zama za mfumo huo wa kiutawala, Bahá'u'lláh, kabla ya kupaa Kwake, kupitia waraka ujulikanao kama ***Kitáb-i-`Ahd* (*Kitabu cha Ahadi)*** aliouandika kwa mkono Wake Mwenyewe, alithibitisha dhima Yake, akawasihi watu wa ulimwengu kutii kile ambacho kitainua daraja lao na kukataza migogoro na ugomvi, na akamteua mwanaye wa kwanza wa kiume aliyeitwa ‘***Tawi Kuu Kabisa’*, (`Abdu'l-Bahá)** kuwa mrithi, mfafanuzi asiyekosea na mfano wa kuigwa katika Imani Yake.




***`Abdu'l-Bahá***

Hali kadhalika, katika Agano na Wasia Wake,**`Abdu'l-Bahá** naye alimteua **Shoghi Effendi,** mjukuu Wake, kuwa mrithi, mfafanuzi na mlezi wa Imani ya Kibahá’i. Shoghi Effendi aliimarisha mfumo huu kwa kuanzisha Asasi (Mashirika) ya kiutawala ndani ya Imani ya Kibahá’i.



***Shoghi Effendi***

## Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

Ni Miaka mia moja baadaye, yaani mnamo 1963, ambapo Wabahá’i wa ulimwengu walichagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ya kwanza. Hili ni Shirika la Juu Kabisa la kiutawala lililoamriwa na Baha’u’lláh katika Imani ya Kibahá’i. Asasi hii ndiyo inayosimamia masuala yote ya Imani kote duniani.



***Makao ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, Haifa, Israel***

Asasi hii ya kipekee—shirika kuu la kwanza kuchaguliwa kiukweli katika historia ya dunia—ndilo linaloisimamia, kuiongoza/kuielekeza na kwa upendo kuishauri jumuiya ya Kibahá'i ya ulimwengu juu ya masuala mbalimbali.



*Makao makuu ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, kwenye miteremko ya Mlima Carmel, Nchi Takatifu, Haifa, Israel.*

## Jinsi gani Wabahá'i Huchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huchaguliwa kila baada ya miaka mitano. Uchaguzi hufanywa katika mazingira tofauti kabisa kuliko aina nyingine yoyote ile ya uchaguzi ulimwenguni. Mashirika yaliyochaguliwa hufanya maamuzi yote ya kisheria katika Imani ya Kibahá'i—Mbahá'i binafsi hana mamlaka, nguvu wala uwezo wowote ule kufanya maamuzi.

Katika ngazi ya kitaifa, kuna Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa ambayo huchaguliwa mara moja kila mwaka na wawakilishi

kutoka sehemu mbalimbali za nchi husika kwenye Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Kitaifa. Wajumbe wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa ndiyo huchagua Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kila baada ya miaka mitano (5) huko katika Nchi Takatifu (Israel).

Na katika ngazi ya mahali (ya chini kabisa), kuna Mabaraza ya Kiroho ya Mahali ambayo pia huchaguliwa na waumini wakaazi wa maeneo husika mara moja kila mwaka ambayo husimamia shughuli za jumuiya katika maeneo yao.

Kuna wajumbe Tisa (9) wanaochaguliwa kwenye kila ngazi ya kiutawala ya Imani. Mchakato huu wa kidemokrasia, na kutokana na ukweli kwamba Wabahá'i hawana kasisi, ndiyo unaohakikisha kwamba Imani ya Kibahá'i hufuata njia unganifu, (ya moja), na huelezea sababu mojawapo kubwa kwa nini Imani ya Kibahá'i imeendelea kubakia moja na iliyounganika na bila migawanyiko takribani karne mbili sasa tangu kuasisiwa kwake.

Chaguzi zote za Kibahá'i ni za Kiroho kwa asili—hakuna kampeni, ugombea, wala aina yoyote ya ushawishi unaofanywa na yeyote. Sala ndiyo kiongozi pekee anayemuwezesha muumini kuwachagua wjumbe sahihi kulingana na sifa bainifu zinazohitajika ili kuweza kuhudumu katika asasi hizi.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ipo kwenye Makao Makuu ya Imani ya Kibahá'i huko Haifa, Israel. Inatunga sheria "ambazo hazijafafanuliwa wazi wazi katika Kitabu, Aqdás." kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu ya Kibahá'i, sheria juu ya masuala ambayo hayakuelezwa katika Maandiko halisi ya **Baha'u'lláh** na **Abdu'l-Baha**:

Yale mambo yenye umuhimu mkuu ambayo hufanya msingi wa Sheria za Mungu yameelezwa wazi wazi katika Maandiko, lakini Nyumba ya Haki ya Ulimwengu imepewa mamlaka kutunga au kufuta sheria saidizi (ndogo ndogo) zinazozitunga. Hekima ya hili ni kwamba nyakati kamwe hazibaki vile vile, kwa kuwa mabadiliko ni sifa ya lazima na muhimu za

ulimwengu huu, na za wakati na mahali. – **Abdu'l-Baha,** imenukuliwa katika *Chemchemi za Uongozi*, uk. 84-86.

Katika Wasia na Agano lake, Abdu'l-Baha aliamuru kwamba Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ya siku zijazo ipo: …chini ya uangalizi na ulinzi wa Uzuri Uliobarikiwa [Baha'u'lláh], chini ya kipaa na uongozi usiokosea wa Yeye Mtakatifu, Aliyetukuka … Chochote wanachoamua kimetokana na Mung…" Wabahá'i wote wameaswa kutii kwa unyenyekevu maamuzi yoyote yanayofanywa na asasi za Imani.



Angalia tovuti ifuatayo ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu kwa maelezo zaidi: universalhouseofjustice.bahai.org.

